**HABARI MUHIMU KUHUSU MANUFAA YA BIMA YAKO YA MEDICAID.**

**Tafadhali Chukua Hatua Mara Moja**

Tunaandika ili kukupa habari muhimu kuhusu manufaa ya bima yako ya Medicaid. Kama inavyohitajika na sheria ya nchi, Jimbo la Rhode Island linatekeleza shughuli ya usasishaji wa ustahiki wa bima ya Medicaid ili kuthibitisha kwamba kila mtu anayepokea bima ya Medicaid anaendelea kustahiki. Rekodi zetu zinaonyesha kwamba una hali maalum zinazoathiri ustahiki wako.

**Muda wa matumizi ya Bima yako ya Medicaid Unaisha**

Maelezo tuliyo nayo yanaonyesha kwamba mapato ya familia yako yanazidi kiwango cha umaskini cha serikali (Federal Poverty Level, FPL) kwa Wazee au Watu Wazima Wenye Ulemavu (Elders or Adults with Disabilities, EAD). Tunatumia FPL ili kusaidia kubainisha ikiwa unastahiki kupokea bima ya Medicaid.

**Unachopaswa Kufanya Ili Uendelee Kupokea Bima ya Medicaid**

Ikiwa mapato ya familia yako yamebadilika, tafadhali tuambie. Unaweza kuripoti mabadiliko ya mapato kwa:

- Kuingia kwenye akaunti yako katika www.healthyrhode.ri.gov. Nenda katika sehemu ya “Report Change” (Ripoti Mabadiliko) ili tueleze kuhusu mabadiliko kwenye mapato yako.
- Kuwasiliana na Idara ya Huduma za Binadamu (Department of Human Services, DHS) ya Rhode Island kwa nambari 1-855-697-4347.

Usichelewe. Tafadhali wasilisha maelezo yaliyosasishwa mara moja ili tuweze kuthibitisha ikiwa unastahiki kuendelea kupokea huduma ya bima.

## Unachoweza Kufanya Ikiwa Mapato Yako Hayajabadilika

Ikiwa mapato yako hayajabadilika lakini una gharama za juu za kila mwezi za huduma ya afya, unaweza kutimiza masharti ya kustahiki kwa mpango wa "spend down". Tutaondoa gharama zako za huduma ya afya kwenye mapato yako kwa kipindi cha miezi sita. Hatua hii inaweza kupunguza mapato yako kwa kiwango cha kutosha ili uweze bado kustahiki kupokea bima ya Medicaid.

Tafadhali hifadhi bili zako zote za matibabu. Tutaangalia kiasi ambacho umetumia baada ya kila miezi sita ili kubainisha ikiwa unatimiza masharti ya mpango wako wa "spend down" na ustahiki kupokea bima ya Medicaid.

Ikiwa una maswali kuhusu kutimiza masharti ya mpango wa "spend down" wa Medicaid, wasiliana na DHS kwa nambari 1-855-697-4347.

## Unachoweza Kufanya Ikiwa Hutimizi Masharti ya Mpango wa 'Spend Down'

Ikiwa hutimizi masharti ya mpango wako wa 'spend down' ya ustahiki wa kupokea bima ya Medicaid, unaweza kuwa na chaguo zingine za kuendelea kupokea huduma ya bima kupitia HealthSource RI (HSRI). Wasiliana na HSRI kuanzia saa 8 a.m. hadi 6 p.m. siku za wiki kwa nambari 1-855-840-4774 ili uzungumze na mtu anayeweza kukusaidia.

Ikiwa hukubali uamuzi wetu kuhusu manufaa yako, unaweza kukata rufaa kwa kufuata utaratibu ulioelezwa kwenye Notisi ya Uamuzi wa Manufaa (Benefit Decision Notice) yako.

Tembelea www.staycovered.ri.gov ili upate maelezo zaidi kuhusu ustahiki wa kupokea bima ya Medicaid na jinsi ya kuomba msaada.